**HOTUBA YA MKUU WA MKOA WA SHINYANGA MHESHIMIWA ZAINAB R. TELACK KWENYE SHEREHE ZA MEI MOSI, 2016 ZILIZOFANYIKA KIMKOA KATIKA HALMASHAURI YA MANISPAA YA SHINYANGA, WILAYANI SHINYANGA TAREHE 01 MEI, 2017.**

***Mwenyekiti wa Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Mkoa,***

***Katibu wa Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Mkoa,***

***Katibu Tawala Mkoa wa Shinyanga,***

***Katibu wa CCM Mkoa,***

***Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya,***

***Wajumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa na Wilaya,***

***Mheshimiwa Mstahiki Meya wa Manispaa ya Shinyanga,***

***Waheshimiwa Wenyeviti wa Halmashauri,***

***Viongozi wa Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Mkoa,***

***Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa,***

***Viongozi wa Idara za Serikali na Taasisi Binafsi,***

***Viongozi wa Vyama vya Wafanyakazi,***

***Viongozi wa Dini,***

***Viongozi wa vyama vya siasa,***

***Wafanyakazi wote kutoka Taasisi mbalimbali na Makampuni binafsi,***

***Waandishi wa Habari,***

***Wageni waalikwa,***

***Mabibi na Mabwana.***

***Habari za Mchana!!!!!***

*Ndugu wafanyakazi,*

Kwa niaba yenu, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa Rehema, kwa kutujalia sisi sote afya njema na kutufikisha mahali hapa salama tukiwa na nguvu za kuendelea kuutumikia Mkoa wetu na Taifa kwa ujumla. Nachukua fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Uongozi wa Shirikisho la vyama vya wafanyakazi Tanzania (TUCTA) ngazi ya Mkoa na Wilaya kwa mandalizi mazuri ya Sherehe hizi za Sikukuu ya Mei Mosi kwa mwaka huu wa 2017, sherehe zimefana sana na watu ni wengi naamini hayo yamewezekana kutokana na maandalizi mazuri mliyoyafanya.

Aidha, kwa namna ya pekee nachukua fursa hii kuwashukuru sana viongozi wa Vyama vya Wafanyakazi Mkoa wa Shinyanga kwa kunialika kuwa mgeni Rasmi katika maadhimisho haya ya Mei Mosi, 2017. Ninayo furaha kubwa kuungana nanyi wafanyakazi wote katika kusherehekea sikukuu hii ya Wafanyakazi kwani Siku hii muhimu hufanyika mara moja tu kwa Mwaka.

***Ndugu wafanyakazi,***

Kama ilivyo kauli mbiu ya maadhimisho ya Mei Mosi kwa mwaka huu ***"UCHUMI WA VIWANDA UZINGATIE HAKI, MASLAHI NA HESHIMA YA WAFANYAKAZI"*** naomba nizungumzie mambo makubwa matatu kama ifuatavyo:

**(i) Uwajibikaji katika kuinua Uchumi**

Serikali yetu chini ya Rais wetu mpendwa ***Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli*** inatekeleza kwa vitendo uwezeshaji wa ujenzi wa viwanda vikubwa na vidogo katika maeneo mbalimbali Nchini. Ili tuendelee kupiga hatua katika hili Wananchi na watumishi wote katika Mkoa wetu tunapaswa kufanya kazi halali kwa bidii kwani Sekta ya viwanda ni mtambuka inayotegemea juhudi za watumishi kutoa huduma bora, wakulima kutoa mazao bora, wafugaji kutoa mifugo bora, wafanyabiashara n.k. Aidha, kwa namna ya pekee nawashukuru sana watanzania wanaoendelea kujituma na kuwekeza katika mkoa wetu. Kwa sasa Mkoa umekuwa kivutio kikubwa cha uwekezaji kwenye sekta ya viwanda; tuna huduma zote muhimu ikiwemo miundombinu imara ya barabara, umeme, maji, amani na utulivu, ukarimu wa wananchi wetu, hakuna urasimu, tuna sheria wezeshi n.k

*"Serikali ya viwanda, inawezekana kila mmoja mahali alipo afanye kazi kwa bidii"*

**(ii) Ulinzi na Usalama.**

Napenda kutumia nafasi hii kuwakumbusha umuhimu wa amani na utulivu kwetu sisi wafanyakazi na Wananchi kwa ujumla, ili kuendana na kauli mbiu ya mwaka huu ni lazima tuwe na Amani. Jukumu la kulinda amani tuliyonayo ni letu sote kwa kushirikiana na Serikali. Naomba nitumie hadhara hii kuwaomba sana wananchi kuwafichua wahamiaji haramu kwani hao ndio wanaoweza kuharibu amani tuliyo nayo kwa kujihusisha na matukio ya kihalifu kwa sababu hawana uzalendo na nchi yetu. Kwa hiyo unapomtilia shaka mtu yeyote tafadhali toa taarifa kwa vyombo vyetu vya usalama ili tuweze kuchukua hatua haraka. ***Wapo wananchi ambao wamewaajiri raia wa kigeni pasipo kufuata utarabu, nawaagiza kuwarudisha kwenye nchi zao mara moja kwa sababu tutaendesha msako ambao ni lazima tutawabaini na hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yao.***

**(iii) Uandikishaji wa watoto walio chini ya umri wa miaka mitano**

Mkoa wetu unaendesha zoezi la kuandikisha watoto walio chini ya umri wa miaka mitano ili waweze kupata vyeti vya kuzaliwa, zoezi hili linafanywa kwenye vituo vya afya na ofisi za watendaji wa kata. Natoa rai kwa wananchi wote kujitokeza kwa wingi ili

kuwaandikisha watoto wetu na kuwawezesha kupata vyeti vya kuzaliwa.

***Ndugu wafanyakazi,***

Nashukuru kwa Risala yenu nzuri ambayo imegusia masuala mengi ikiwemo kuipongeza Serikali kwa jitihada inayoendelea nayo ya kusogeza huduma muhimu kwa wananchi hususani huduma za afya.

Aidha, Nimeisikiliza Risala yenu kwa umakini mkubwa sana na kuzisikia changamoto zote zinazowakabili, naahidi kuzipokea changamoto zenu zote zinazohitaji utatuzi wa ngazi ya Taifa na kuziwasilisha kwa Mamlaka husika ili zifanyiwe kazi mapema iwezekenavyo, kwa zile zinazohitaji utatuzi wa ngazi ya Mkoa, Wilaya na Mamlaka za serikali za mitaa nitazifanyia kazi mwenyewe:

*Kuhusu suala la Sekta binafsi kutotoa mikataba ya ajira, kuwazuia wafanyakazi kutojiunga na vyama vya wafanyakazi, kutotoa hati za malipo ya mishahara, kutolipa michango ya wafanyakazi kwenye mifuko ya kijamii, kutotoa likizo zote za kisheria, kutozingatia masaa tisa ya muda wa kazi au kutolipa fedha za masaa ya ziada ya kazi (extra duty) na kutotoa vitendea kazi.*

Mkoa umekuwa ukiwaagiza mara kwa mara waajiri wote wa Sekta binafsi kuhakikisha kwamba wanazingatia sheria na kanuni za uajiri kwa watumishi wao. Ikumbukwe pia kuwa *Suala la*

*Waajiri kuwazuia Wafanyakazi kujiunga na vyama vya wafanyakazi ni kinyume cha Sheria ya Ajira na Mahusiano kazini Na. 6 ya Mwaka 2004 kifungu cha 9 (1) (a) na (b) ambayo inawapa haki watumishi kujiunga na vyama vya wafanyakazi.*

***Naagiza waajiri wote wa sekta binafsi kufuata sheria za kazi na kuondoa mapungufu hayo ndani ya wiki mbii kuanzia tarehe ya leo. Tarehe 15 Mei, 2017 katibu Tawala wa Mkoa uunde timu maalumu itakayowahusisha Makatibu Tawala wa Wilaya, wawakilishi wa vyama vya wafanyakazi na Ofisi ya kazi Mkoa ili wazipitie sekta binafsi zote hususani hizo zilizobainishwa na Shirikisho la vyama vya wafanyakazi kama zimetekeleza agizo langu. Endapo hawatatekeleza kwa vitendo sio maneno nitachukua hatua kali za kisheria dhidi yao.***

***Ndugu wafanyakazi,***

Natoa Rai kwa Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi kuendelea kutoa ushirikiano chanya kwa Serikali na wafanyakazi ili wafanye kazi kwa kujituma pasipo mazoea. Pia, muwaelimishe Wafanyakazi kutumia muda wao mwingi katika vituo vyao vya kazi ili kuongeza ufanisi katika kuwatumikia Wananchi wetu.

Ushauri wangu kwa Viongozi wa Vyama vya Wafanyakazi ni kwamba, mnao wajibu wa kuhakikisha kuwa mnaongeza idadi ya wafanyakazi katika vyama vyenu kwa kuweka mikakati thabiti ya kuwatembelea Wafanyakazi kazi wapya ikiwa ni pamoja na kutengeneza uhusiano mzuri kati yenu na waajiri

katika Taasisi zote za Umma na Binafsi. Serikali ngazi ya Taifa, Mkoa na Wilaya inaendelea na jitihada zilizopo za kutafuta wawekezaji wakubwa na wadogo kutoka ndani na nje ya Nchi katika Sekta ya viwanda vitakavyotumia malighafi zinazotokana na kilimo na mifugo ili kuongeza wigo wa upatikanaji wa ajira kwa Wananchi wa Mkoa wetu na Taifa kwa ujumla. Hamna budi kuendelea kuiunga mkono Serikali katika jitihada za kuinua Uchumi wa Mkoa kwa kuwaletea Wananchi maendeleo.

***Ndugu wafanyakazi,***

Kwa mara nyingine tena nawaahidi kwamba yale yote mliyo yawasilisha kwangu kupitia Risala yenu nitayafanyia kazi ikiwemo kuwasilisha kwenye mamlaka husika, ikumbukwe kwamba yapo mambo ambayo Mkoa hauna mamlaka nayo hivyo ni jukumu letu kuhakikisha kwamba yanafika katika mamlaka husika na kupatiwa ufumbuzi.

***Sote kwa pamoja tuendelee kutumia fursa nyingi zilizopo katika Mkoa wetu kwa ajili ya kujiletea maendeleo na kwa kufanya hivyo tutatekeleza kwa vitendo falsafa ya Serikali ya Awamu ya tano yaani "Hapa Kazi Tu"***

***"UCHUMI WA VIWANDA UZINGATIE HAKI, MASLAHI NA HESHIMA YA WAFANYAKAZI"***

**MEI MOSI OYEEEE!!!!!!!!!!**

***Nawatakieni sikukuu njema.***

**AHSANTENI SANA KWA KUNISIKILIZA**